



## DCB Commercial Bank Plc

### TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI NA MBILI WA MWAKA

Taarifa inatolewa kwamba, Mkutano Mkuu wa Ishirini na Mbili wa mwaka wa DCB Commercial Bank Plc, utafanyika siku ya Jumamosi tarehe 14 Septemba 2024 kwa njia ya mtandao, kuanzia saa nne kamili (4:00) asubuhi.

#### Agenda

1. Kuthibitisha akidi na kufungua mkutano Mkuu wa 22 wa mwaka
2. Kuridhia agenda ya Mkutano Mkuu wa 22 wa mwaka
3. Kuthibitisha kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa 21 wa mwaka
4. Kupokea na kuridhia utekelezaji wa yatoanayo na Mkutano Mkuu wa 21 wa mwaka
5. Kupokea na kuridhia taarifa za Bodi ya Wakurugenzi na hesabu zilizokaguliwa za Mwaka 2023
  - 5.1 Taarifa ya wakurugenzi ya mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba, 2023
  - 5.2 Taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba, 2023
  - 5.3 Taarifa ya mkaguzi huru ya hesabu zilizokaguliwa za mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba, 2023
6. Kupokea na kuidhinisha pendekezo la kuongeza mtaji wa benki kwa njia ya hisa stahiki
7. Kupokea taarifa ya Kuisha kwa muda, Kuongeza muda na uteuzi wa wajumbe wa Bodi
8. Kuteua mkaguzi huru wa hesabu kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 31 Disemba 2024
9. Kupokea na kuridhia pendekezo la malipo ya ada kwa wajumbe wa bodi
10. Kupanga tarehe ya Mkutano Mkuu wa 23 wa mwaka
11. Mengineyo
12. Kufunga mkutano

#### MAELEZO

1. Wanahisa wanaotarajia kuhudhuria mkutano mkuu wanatakiwa wawe na CDS namba ambazo zinapatikana kwenye risiti ya uwekezaji wa hisa (depository receipt) au taarifa ya akaunti (CSDR account statement).
2. Wanahisa ambao hawataweza kuhudhuria Mkutano wanaruhusiwa kuchagua wawakilishi watakaohudhuria na kupiga kura kwa niaba yao kwa kufuata/kuzingatia sheria na Katiba ya Kampuni. Fomu ya uwakilishi (Proxy Form) lazima ijazwe na kuwasilishwa kwenye ofisi ya Katibu wa Benki iliyopo Makao Makuu ya Benki ya DCB au kwa njia ya mtandao kupitia barua pepe [shareholder@dcb.co.tz](mailto:shareholder@dcb.co.tz) au matawini kabla ya saa 4 asubuhi siku ya Ijumaa tarehe 13 Septemba 2024.
3. Nakala za taarifa ya mwaka na fomu za mwakilishi (proxy forms) zitapatikana matawini na kwenye tovuti ya benki ([www.dcb.co.tz](http://www.dcb.co.tz)).
4. Kufungwa kwa orodha (Register) ya wanahisa - tarehe 11 Septemba 2024
5. Mapendekezo ya wanahisa yawasilishwe kwenye ofisi za makao makuu zilizoko jengo la DCB Magomeni Mwembechai au kwa barua pepe kabla ya saa 8.00 mchana siku ya Alhamisi tarehe 12 Septemba 2024.

#### KWA IDHINI YA BODI,

**Regina Mduma**  
**Katibu wa Kampuni**  
**Agosti 2024.**